Cambridge Assessment International Education

# Cambridge IGCSE™

CANDIDATE NAME

CENTRE NUMBER

CANDIDATE NUMBER

* 0 1 2 3 4 5 6 7 8 9 *

**SWAHILI** **0262/01**

Paper 1 Reading and Writing **For examination from 2021**

SPECIMEN PAPER **2 hours**

You must answer on the question paper.

No additional materials are needed.

**INSTRUCTIONS**

- Answer **all** questions.
- Use a black or dark blue pen.
- Write your name, centre number and candidate number in the boxes at the top of the page.
- Write your answer to each question in the space provided.
- Do **not** use an erasable pen or correction fluid.
- Do **not** write on any bar codes.
- Dictionaries are **not** allowed.

**INFORMATION**

- The total mark for this paper is 60.
- The number of marks for each question or part question is shown in brackets [ ].

This document has **14** pages. Blank pages are indicated.

© UCLES 2018

## Zoezi 1

Soma kifungu kifuatacho kuhusu mwanzilishi wa kampuni ya uchapishaji, na halafu jibu maswali yanayofuata.

Salome Labeja ni mwanzilishi wa *Hadithi Tamu*, kampuni ya uchapishaji inayowawezesha waandishi Waganda kuonyesha ubunifu wao. Kampuni hii imechapisha riwaya mbili pamoja na hadithi fupi nyingi. Ilianza kama blogu ndogo aliyoitengeneza pamoja na mume wake mwaka 2014. Hivi sasa kuna wafanyakazi wanne na kampuni imejipatia sifa nzuri ndani ya sekta ya uchapishaji.

Tangu alipokuwa kijana, Salome alivutiwa na uandishi. Ndiyo maana alichagua kuwa mwandishi wa habari baada ya kuhitimu masomo yake. Baada ya muda mfupi, alikutana na waandishi wengi wenye kipaji ambao hawakuweza kuchapisha kazi zao. Akapata hamu ya kuwasaidia na hivyo kupata fursa ya kutoa mchango wa maana. Akawa na ndoto ya kuanzisha kampuni yake mwenyewe ya uchapishaji ili kuwawezesha waandishi kueneza kazi zao. Lakini alikuwa na kikwazo kimoja, nacho ni mahitaji ya kazi yake ya kila siku.

'Niliipenda kazi yangu ya uandishi wa habari. Mshahara ulikuwa wa kutosha na nilijifunza mambo mengi. Lakini ilinichokesha pia. Nilitarajiwa kubaki ofisini mpaka usiku na sikuwa na wakati wala nguvu ya kutosha kufuatilia mambo yangu mengine. Hivyo, nilikata shauri kuacha kazi na kujaribu kutimiza ndoto yangu.'

Baada ya kuacha kazi, Salome alijitolea kufanya kazi katika kampuni mashuhuri iliyopo Afrika ya Kusini ili kupata uzoefu wa kufanya biashara. Kulikuwa na faida ambazo hakuzitarajia. Kwa mfano, alipokuwa huko, aliweza kujenga mahusiano ya kikazi na wachapishaji wengine kutoka sehemu tofauti za bara la Afrika.

'Kuwa Afrika ya Kusini kulinitia mori. Niliporudi Uganda nilianza kujitahidi sana. Nilifanya mahojiano na waandishi tofauti, niliandika makala na kuhudhuria shughuli kadhaa. Sikupata mshahara wowote lakini nilipata furaha ya kipekee kufanya kazi niliyoipenda na nikafarajika sana.'

*Hadithi Tamu* imejitwika wajibu wa kuchangia kuimarisha utamaduni wa kusoma nchini Uganda kwa kupitia vikundi vya kusoma vitabu. Katika kikundi kimoja kinachoitwa *Jikoni* kilichopo jijini Kampala, watoto wenye umri wa kuanzia miaka minne hadi miaka kumi na mbili wanakusanyika kusoma vitabu pamoja. Siku hizi kuna zaidi ya watoto 45 katika kila kikundi. Kwa sababu ya jitihada kama hizi watoto na watu wazima wengi zaidi wameanza kupenda kusoma vitabu na fasihi.

'Vikundi hivi vya kusoma vitabu vimesababisha ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaosoma Uganda. Kweli tumeona matokeo makubwa. Wazazi wameshangaa jinsi watoto wao walivyobadilika. Watoto wengi waliokuwa hawapendi kuzungumza na wenzao wamekuwa wa kwanza kujitokeza kwenye kusoma kwa sauti. Wazazi wengine wanatuambia kwamba watoto wao wanavutiwa sana na vitabu sasa, ingawa awali hawakuwa na hamu ya kusoma hata gazeti. Kusikia hivyo kunanifanya nijivunie juhudi zetu.'

© UCLES 2018 

1 Nani aliyemsaidia Salome kuanzisha kampuni yake?

.............................................................................................................................................. [1]

2 Jambo gani lilimkera Salome kuhusu hali ya waandishi aliokutana nao?

.............................................................................................................................................. [1]

3 Kazi ya Salome ilimzuia vipi kutimiza ndoto yake kuwa mchapishaji?
Taja sababu **mbili.**

..................................................................................................................................................

.............................................................................................................................................. [2]

4 Kwa nini Salome alikwenda nje ya nchi?

.............................................................................................................................................. [1]

5 Vikundi vya kusoma vina lengo gani?

.............................................................................................................................................. [1]

6 Tunajuaje kwamba vikundi vya kusoma vimewafanya watoto kuwa wanajiamini zaidi?

.............................................................................................................................................. [1]

7 Kutokana na kifungu hiki, tunajuaje kwamba kutengeneza pesa si muhimu sana katika bidii za Salome?

.............................................................................................................................................. [1]

[Jumla: 8]

## Zoezi 2

Wanandondi wanne wa kike wanaelezea jinsi walivyoingia katika mchezo huo.

### A Asha

Nilianza kupigana ndondi katika kijiji kidogo ambapo nilizaliwa. Nilipokuwa msichana nilikuwa nikicheza na wavulana na nilipendelea michezo yao kuliko michezo ya wasichana. Nilipokuwa na miaka kumi na mbili niliamua kuijiunga na kikundi kidogo cha ndondi kijijini kwangu. Nilianza mazoezi ya ndondi na nilisifiwa sana na makocha wangu. Baada ya muda si mrefu, nilipendekezwa kujiunga na timu ya taifa na kualikwa kuwa nao huko mji mkuu. Kusema kweli, sikuwa na huzuni wala hofu kuhama nyumbani. Hali ya huduma kijijini ilikuwa ni mbaya sana … hata hatukuwa na ulingo wa kufaa. Nilipofika mji mkuu niliweza kushinda tuzo ndani ya mwaka mmoja tu. Kwa sababu hiyo, nilichaguliwa kuhusika kwenye mashindano huko Ulaya. Nilipata tuzo kule pia! Ninaupenda mchezo huu.

### B Jorbelle

Kila watu wanapofikiria mchezo wa ndondi hapa, wanamfikiria mwanandondi mashuhuri Muhammad Ali. Lakini kwa mimi mwenyewe alikuwa mwanandondi mwengine anayejulikana sasa, Mike Tyson, ambaye alinifanya nitake kupigana. Nilimpenda sana nilipokuwa mtoto na ninaamini nitakuwa mrefu na hodari kama alivyokuwa yeye. Tayari kama ungeniona ulingoni usingejua nani ni nani – Tyson au Jorbelle! Kitu kinachonichochea sasa ni kuwa mtu mwema zaidi kuliko mimi nilivyo leo. Ninaamini kwamba nikijitahidi sana, maisha yangu yatakuwa mazuri zaidi na siku moja nitajulikana duniani kote. Kupigana ndondi ni kazi yangu. Sina nyingine. Siwezi kumtegemea mtu mwingine kwa kazi, hata kama mshahara wangu ni mdogo. Fikra za pesa au kazi si muhumu sasa kwani nimekazia fikra na nguvu zangu zote kwenye nia ya kushinda matuzo. Sina mume wala mtoto. Familia yangu ni mama yangu na bibi yangu tu. Hakuna cha kunirudisha nyuma!

### C Safia

Nimekuwa nikipigana ndondi kwa miaka mitano sasa. Hamna mtu ye yote aliyenidokezea kuhusu ndondi au aliyenitia moyo. Kuanza ndondi kulikuwa ni ndoto yangu mwenyewe. Nilijijenga kinguvu na kiuwezo. Kuna wasichana watano tu wanaopigana kwenye kikundi chetu, na tunapaswa kujitahidi sana. Ni wasichana wachache sana watakaochaguliwa kushindana katika mashindano ya barani. Ni vigumu sana, lakini ukiwa na hamu ya kutosha utaweza kufanya cho chote na kufanikiwa. Nilishinda tuzo langu la kwanza mwaka uliopita. Kushinda kulinisisimua sana na kulinifanya nijiamini zaidi. Ningependa kutunukiwa zaidi kipesa kwa mafanikio yangu. Hivi sasa malipo ni madogo sana, ingawa kazi yenyewe ni ngumu. Kazi ya kuwa mchezaji ndondi haidumu sana. Sijui nitafanya nini baadaye, kwa sababu sitaki kuwa kocha. Lakini, kwa sasa nimeridhika kupigana kwa ajili ya upendo wangu mwenyewe wa mchezo huu. Nitajaribu kushinda matuzo mengi iwezekanavyo.

### D Zawadi

Kupigana ndondi ni shauku yangu. Ninatarajia kuwa bingwa wa dunia. Nilianza bila kukusudia. Nilikuwa ninasoma sheria chuoni katika mji mkuu na nilikuwa nikikimbia kwa ajili ya mazoezi tu. Hakukuwa na kikundi cha kukimbia chuoni, hivyo nilianza kukimbia pamoja na kikundi cha ndondi. Halafu walinishawishi kujiunga nao. Kwanza mazoezi yalikuwa magumu sana. Kocha alikuwa mzuri sana, lakini nilikuwa msichana pekee na hivyo nilipata changamoto nyingi. Lakini kocha aliona uwezo wangu na kunitia moyo sana. Halafu alipendekeza jina langu kwa timu ya taifa pia. Niliogopa sana nilipoingia ulingoni kwa mara ya kwanza, baada ya miezi minne ya mazoezi tu, na nilishindwa. Ilinichukua miezi minane kabla ya kuwahi kushinda kwa mara ya kwanza. Sasa ninaamini nina uwezo wa kutosha kushinda tuzo, lakini ningekuwa na nafasi kubwa zaidi ningeweza kupata mafunzo nje ya nchi. Hapa huduma si nzuri sana na ninapaswa kufanya mazoezi nje, kando ya njia kuu.

© UCLES 2018

Soma taarifa (**8–16**) zifuatazo. Weka alama ya tiki (✓) kwenye kisanduku kuonyesha aya (**A–D**) inayohusiana na kila taarifa. Kuna mfano mmoja hapa chini.

**Mfano**

Mwanandondi yupi …

alihamia mahali pengine kujiunga na timu ya taifa?

**A** ✓ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐

**8** anataja kwamba angependelea kupata fedha zaidi?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**9** amepigana ndondi katika bara lingine?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**10** hakuweza kushinda katika mechi yake ya kwanza?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**11** anataka kuhamia nje kwa ajili ya maendeleo yake?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**12** anafikiria atakachofanya baada ya kustaafu?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**13** alijihusisha na ndondi kwa bahati?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**14** anataka kutumia ndondi kuboresha utu wake?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**15** anajilinganisha na mtu maarufu katika mchezo wa ndondi?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

**16** alipaswa kuvumilia huduma mbaya alipoingia ndondini?

**A** ☐ **B** ☐ **C** ☐ **D** ☐ [1]

[Jumla: 9]

© UCLES 2018

**BLANK PAGE**

© UCLES 2018

**Zoezi 3**

Soma makala yafuatayo kuhusu matumizi ya simu za mikononi darasani.

Kweli wanafunzi wa leo ni wenyeji wa enzi za kiteknolojia. Kulingana na utafiti uliochapishwa mwaka uliopita, vijana watatu kati ya wanne siku hizi wana simu za kisasa na wengi wanazileta shuleni kila siku. Lakini je, ni wazo zuri kuwaruhusu wanafunzi walete au watumie simu zao darasani? Tulizungumza na walimu, wanafunzi na wazazi kufahamu zaidi.

Farouk ni mwalimu wa hesabu katika shule ya kimataifa Kampala. Alianza kufundisha miaka kumi iliyopita, wakati ambapo hakukuwa na wanafunzi wo wote wenye simu. Anaona kwamba simu zinaweza kuwasaidia walimu, kwa mfano kusambaza taarifa na kuwatumia wanafunzi mazoezi ya kazi za nyumbani. Lakini anataka wanafunzi wasiruhusiwe kabisa kuzileta darasani. 'Kwangu, simu darasani ni hatari tu. Kwanza, zinawawezesha wanafunzi kuibia katika mitihani, na kweli tatizo hili limeenea sana hivi sasa. Pia wanafunzi wenye simu hawasikilizi darasani na hukengeushwa nazo mara nyingi. Darasani ni kazi ya wanafunzi kusikiliza na kusoma, na ni kazi ya mwalimu kuhakikisha kwamba hakuna fujo. Kwa maoni yangu simu ni kipingamizi tu.'

Khadija na Jonathan wanaishi Moshi na ni rafiki wa miaka mingi. Wote wawili wanasoma kwenye shule moja ya sekondari Moshi. Jonathan ana miaka kumi na mitano, na anapenda sana masomo ya sanaa. Hakubali kwamba matumizi ya simu za mikononi huleta shida darasani, bali anafikiri shida ni walimu wasiojaribu kufanya madarasa yawapendeze wanafunzi. 'Ninampenda sana mwalimu wangu wa sanaa – madarasa yake ni ya kuvutia na sina haja ya kuangalia simu yangu. Lakini walimu wengine wanaongea tu na ni vigumu kukaa na kusikiliza kwa masaa mengi mfululizo.'

Khadija anacheka na kuzungusha macho kwa mzaha. Yeye ni msichana mwenye umri wa miaka kumi na minne, na ni mwanafunzi hodari aliyetunukiwa Tuzo la Darasa mwaka uliopita. Mama yake alimnunulia simu kama zawadi kwa kupata Tuzo hilo. Khadija anakubali si shida kubwa kutumia simu darasani, lakini bora uzitumie kusaidia ufahamu wako – sio kujikengeusha tu. 'Simu yangu ya kisasa inanisaidia kupata majibu kwa urahisi zaidi. Sasa sihitaji kumwuliza mwalimu maswali na ninaweza kufahamu zaidi muktadha wa mada zinazofundishwa. Kwa mfano, juzi tulikuwa tukisoma kuhusu Azimio la Arusha na niliweza kupitia makala na magazeti pale pale nilipokaa darasani!'

Mama Khadija alikuwa na hofu kidogo alipomnunulia mtoto wake simu, kwa sababu wazazi wengi walikuwa wamemlalamikia kuhusu athari za simu za kisasa kwa watoto wao. 'Wengi waliniambia kwamba alama zao zilishuka mno. Wanalalamika kwamba watoto wao hawataki kufanya kazi zao za nyumbani, bali wanapendelea kutumia masaa kwenye mitandao ya kijamii au kucheza michezo ya simuni tu.' Lakini anasema bado hajaona athari mbaya kwa Khadija. 'Alama zake bado ni za juu, na hutumia simu yake kusambaza taarifa kati yake na rafiki zake kwenye vikundi vyao vya masomo ya shule. Pia sasa simu ni sehemu ya maisha tu na usipoweza kuzitumia utapitwa na wakati. Sijamwekea masharti yo yote, na nimeona ameitumia kwa makini.' Khadija anatabasamu na kuongeza: 'Kwa kweli, nilishukuru jinsi mamangu alivyoniamini na nilitaka kumthibitishia kwamba alikuwa sahihi. Kwa hivyo, nimekuwa nikitumia simu kwa uangalifu.'

Mwalimu Ida Hamdani alianza kufundisha miezi sita iliyopita. Yeye hakutaka kupiga marufuku simu darasani. Bali, amegundua kwamba simu zinaweza kuwa chombo cha kuboresha mazingira ya masomo darasani kwa wanafunzi na walimu pia, mradi tu unasimamia jinsi zinavyotumiwa. Kwake, hali halisi ni kwamba vijana hutumia simu kila siku, tena watapaswa kuzitumia katika maisha yao yajayo, na ni wajibu wa walimu kuwasaidia kuzitumia kwa njia sahihi. 'Kitu cha muhimu ni kuweka sheria kwa matumizi ya simu darasani, pamoja na kueleza wazi wanafunzi watakavyoathirika zikitumiwa vibaya. Ukijaribu kuwazuia wanafunzi wasitumie simu kabisa, wataasi tu, lakini ukishirikiana nao kuhakikisha kwamba wanazitumia kwa njia nzuri, watakubali.'

© UCLES 2018

Andika maelezo mafupi chini ya vichwa vya habari (**17–20**) vinavyotokana na makala uliyoyasoma.

**17** Fikra za vijana kuhusu matumizi ya simu za mikononi darasani.

- ..........................................................................................................................................
- ..........................................................................................................................................
- .......................................................................................................................................... [3]

**18** Hofu za wazazi kuhusu matumizi ya simu za mikononi kwa watoto wao.

- ..........................................................................................................................................
- .......................................................................................................................................... [2]

**19** Faida kwa walimu kutumia simu kama kifaa cha kufundishia.

- ..........................................................................................................................................
- .......................................................................................................................................... [2]

**20** Fikra za walimu kuhusu jinsi ya kushughulikia matumizi ya simu darasani.

- ..........................................................................................................................................
- .......................................................................................................................................... [2]

[Jumla: 9]

Katika **zoezi 4**, utatumia maelezo haya kutunga ufupisho.

## Zoezi 4

Makala ya zoezi 3 yanazungumzia matumizi ya simu za mikononi darasani.

**21** Sasa tunga ufupisho wa maoni ya watu wazima kuhusu matumizi ya simu darasani. Unaweza kutumia maelezo yako mengine kutoka zoezi 3 ili kukusaidia.

Ufupisho wako usizidi **maneno 100**.

Tumia maneno yako mwenyewe kadiri iwezekanavyo.

Utapata alama zisizozidi 4 kwa maudhui ya ufupisho wako, na alama zisizozidi 6 kwa lugha makini na sahihi.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

[Jumla: 10]

© UCLES 2018

**Zoezi 5**

**22** Mwezi ujao rafiki yako kutoka nchi za nje atakutembelea. Ni mara yake ya kwanza kutembelea nchi yako. Andika barua pepe kumweleza pahala muhimu ambapo apatembelee atakapokuwa nchini. Katika barua yako ya pepe unapaswa kutaja:

- Pahala hapo pakoje
- Umepajuaje pahala hapo
- Pahala hapo pana umuhimu gani kwako

Barua yako ya pepe isizidi **maneno 120**.

Utapata alama zisizozidi 3 kwa maudhui ya barua yako ya pepe, na alama zisizozidi 5 kwa mtindo na umakini wa matumizi ya lugha yako.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

[Jumla: 8]


© UCLES 2018

## Zoezi 6

**23 'Wanafunzi wote wanatakiwa kutumia siku moja kila wiki kwa kufanya kazi za kujitolea.'**

Je, unakubaliana na wazo hili?

Andika makala katika gazeti la shule ili kutoa maoni yako. Makala yasizidi **maneno 200**.




Unaweza kutumia maoni ya hapo juu, na pia ni lazima kutumia mawazo yako mwenyewe.

Utapata alama zisizozidi 8 kwa maudhui ya makala, na alama zisizozidi 8 kwa mtindo na umakini wa matumizi ya lugha yako.

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

[Jumla: 16]

**BLANK PAGE**

*Copyright Acknowledgements:*

Exercise 1: © Ibrahim Batambuze; *How Kakoma Is Creating A Generation Of Book Readers Right From The Grass Roots*; This is Uganda; May 15 2018.
Exercise 2: © Hugh Kinsella Cunningham; *Fight like a girl: the female boxers of the Democratic Republic of the Congo*; The Guardian; 14 July 2017.

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (UCLES) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

Cambridge Assessment International Education is part of the Cambridge Assessment Group. Cambridge Assessment is the brand name of the University of Cambridge Local Examinations Syndicate (UCLES), which itself is a department of the University of Cambridge.